TANGAZO LA SERIKALI Na. 218 la tarehe 29/3/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)

(SURA YA 288)

# SHERIA NDOGO

SHERIA NDOGO YA MJI WA KIHISTORIA WA MIKINDANI NA MAENEO MENGINE YA URITHI YALIYOHIFADHIWAYA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MTWARA-MIKINDANI YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Mji wa Kihistoria wa Mikindani na maeneo mengine ya urithi yaliyohifadhiwa ya Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani za Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa yaMtwara–Mikindani.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii isipokwa pale Muktadha utahitaji vinginevyo: -

"eneo la Hifadhi ya Urithi" maana yake eneo lote lilioainishwa na Halmashauri lililotengwa maalum kwa madhumuni ya Uhifadhi wa Urithi wa kiutamadauni;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara – Mikindani;

"jengo la nyongeza" maana yake ni maboresho katika eneo ambalo matumizi au matumizi yaliyokusudiwa ni saidizi kwa jengo kuu linalopatikana katika eneo hilo;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria hii;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa

Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara – Mikindani au Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"shughuli zilizokatazwa" maana yake ni upanuzi, umaliziaji, kazi za ujenzi, ubomoaji, uwekaji alama, ukarabati, kazi za kimuundo, kazi za usanifu na kazi nyingine zozote zinayofanyika bila ruhusa ya mkurugenzi kwa madhumuni ya uhifadhi chini ya Sheria hii;

"mambo ya kale" inajumusiha majenzi, masalia na mikusanyo iliyohifadhiwa;

"mikusanyo ya kiethnografia" maana yake ni mkusanyo wowote unaohamishika uliotengenezwa, kuundwa, kupakwa rangi, kuchongwa, kuandikwa au vinginevyo kuzalishwa au kuboreshwa na mwanadamu, katika Tanzania baada ya mwaka 1863, kwa matumizi katika shughuli yoyote ya kijamii au ya kiutamaduni, iwe au bado unatumiwa na jamii yoyote katika Tanzania, ila haijumuishi mkusanyo wowote uliotengenezwa, kuundwa, kupakwa rangi, kuchongwa, kuandikwa au vinginevyo kuzalishwa au kuboreshwa na mwanadamu kwa ajili ya kuuzwa kama ukumbusho;

"Majenzi ya kihistoria" maana yake ni na yanajumuisha-

(a) Jengo lolote, ngome, "interment", "midden", bwawa, au muundo wowote ulioinuliwa, kujengwa au kuundwa na mwanadamu katika Tanzania kabla ya mwaka 1863;

(b) Michoro yoyote ya mapangoni au mkusanyo mwingine wowote usiohamishika, kuchongwa sanamu, kuchongwa, kukatwa, au kuboreshwa na mwanadamu katika Tanzania kabla ya mwaka 1863;

(c) boma la udongo (earth work), mfereji, mlango wa kuingilia, kisima, pango, handaki au

maboresho mengine yoyote, ya kuchimba udongo au miamba, yaliyochimbwa au yaliyobuniwa vinginevyo na mwandamu katika Tanzania kabla ya mwaka 1863, iwe au la majenzi yaliyoboreshwa, kuongezewa au kurejeshwa katika tarehe ya mbele na iwe au limejumuishwa katika orodha iliyochapishwa na Mkurugenzi wa Mambo ya Kale;

(d) eneo au muundo wowote usiohamishika uliotangazwa kuwa mkusanyo wa kihistoria chini ya kifungu cha 3 cha Sheria ya Malikale;

Sura 333

(e) ardhi inayoungana kama inavyoweza kuhitajika kwa dhumuni la uzio, kufunika au vinginevyo kuhifadhi majenzi ya kihistoria;

"makumbusho" maana yake ni taasisi za kielimu na kiutamadumi kwa ajili ya ukusanyaji, uhifadhi na utafiti wa vitu vya kisayansi na kiutamaduni;

"mikusanyo iliyohifadhiwa" maana yake ni mkusanyo wowote wa kiethnografia au mlango wa mbao au fremu yoyote ya mlango iliyochongwa katika Tanzania, katika mtindo wa kiafrika au wa kiutamaduni kabla ya mwaka 1940;

"masalia" maana yake ni mkusanyo wowote unaohamishika uliotengenezwa, kuundwa, kupakwa rangi, kuchongwa, kuandikwa au vinginevyo kuzalishwa au kuboreshwa na mwanadamu, katika Tanzania baada ya mwaka 1863, iwe au umeboreshwa, kuongezewa au kurejeshwa katika tarehe ya mbele na inajumusha mwanadamu, au viumbe wengine wenye uti wa mgongo, visukuku au mabaki yoyote ya wanyama na mimea, inayopatikana katika Tanzania;

"sifa za usanifu" maana yake ni upande, ukuta, nyuso za kuta kona za bodi, mabano, nguzo, nguzo chomozi, madirisha milango, mazingira ya dirisha na mlango au wigo wa mlango, mchomozo,

zinara, kenchi pambo, uzio na mapambo, umaliziaji, rangi, vifaa vyake vya usanifu na sifa sawa zingine zote za nje;

"sura" inajumuisha sifa za usanifu na za sura ya nchi;

"vibali vya ukarabati" maana yake ni kibali kilichoidhinishwa na Makumbusho ya Taifa ya Tanzania na ikiwa kuna ulazima anaweza kumtaarifu Mkurugenzi baada ya kutoa kibali;

"sifa za sura ya Nchi" maana yake ni uzio, ukuta wa kuzuia, chemchemi, baraza, mfereji, sanamu, au sifa zingine, ambazo zinapatikana katika eneo na nje ya kuta za nje za jengo;

"thamani ya urithi" maana yake ni thamani au manufaa ya mali ya kijamii, kihistoria, kiutamaduni, kiusanifu, kisayansi au kielimu au umuhimu wa matumizi yake; na

Mikusanyo iliyoorodheshwa

4. Kwa madhumuni ya uhifadhi chini ya Sheria hii majengo yote, miundombinu, majengo ya kihistoria, majenzi, masalia, mikusanyo na maeneo mengine chini ya Sheria hii yameainishwa kuwa na thamani ya urithi na kwa hiyo yanahifadhiwa kwa mujibu wa Sheria hii.

Uhifadhi wa Urithi

5. Hakuna mtu, watu au kundi la watu, shirika, taasisi au chombo kingine cha aina yoyote kitakachoweza kutekeleza, kufanya au kitasababisha kutekelezwa au kufanyika shughuli zilizokatazwa katika eneo la hifadhi la mji wa kihistoria wa Mikindani au eneo lingine lolote ndani ya Halmashauri ambalo limeainishwa kama eneo la urithi isipokuwa kama shughuli hizo, au matendo mengine yameidhinishwa na Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa.

Makatazo

6. Hakuna mtu yeyote, kikundi cha watu au taasisi atakayeruhusiwa kufanya yafuatayo ndani ya maeneo ya urithi yaliyohifadhiwa:

(a) kubomoa, au kuruhusu kuharibu au kuruhusu kubomolewa kwa jengo, muundo au

muonekano ambao uko katika eneo la hifadhi ya urithi au jengo, muundo au muonekano ambao ni mali ya urithi uliyohifadhiwa;

(b) kujenga, au kuruhusu kuharibu au kuruhusu ujenzi wa jengo, muundo ambao uko katika eneo la hifadhi ya urithi;

(c) kukarabati jengo kwa kutumia vifaa vingine tofauti na vifaa vya asili

(d) kutupa taka za aina yoyote isipokuwa katika kasha lililotolewa kwa ajili hiyo;

(e) kuteketeza, kuharibu, kujeruhi, kuchana au kuondoa mti, kichaka, nyasi au uoto mwingine uliopo;

(f) kuharibu, kuchana au kuondoa ubao wa matangazo, alama ya ishara au jengo lolote au muundo wowote uliojengwa kihalali;

(g) kuondoa au kwa namna yoyote kuharibu mwamba wowote kutoka sehemu yake ya asili;

(h) kuhamisha au kwa namna yoyote kuharibu kitu chochote kiwe cha bandia au si cha bandia kutoka sehemu yake sahihi;

(i) kusababisha moto kwenye nyasi, mimea ya chini au miti ya eneo linalozunguka; na

(j) kusababisha au kufanya maandishi ya aina yoyote;

Fidia

7. Mkurugenzi wa Manispaa au Afisa yeyote aliyeidhinishwa hawatakabiliwa kwa kitendo au mienendo mingine yoyote kuhusiana na kitendo chochote alichofanya, au hakufanya ambacho hakijasababishwa na zembe wakati wa utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Sheria hii.

Thamani ya Urithi

8. Kwa dhumuni la kuamua kama jengo, muonekano, mali, eneo au sehemu inaweza kuwa na tabia za urithi au thamani ya urithi chini ya sheria ndogo hizi,

Mkururgenzi anaweza kuzingatia yafuatayo:

(a) usanifu, historia, utamaduni, jamii au kiimani umuhimu au ubora wa jengo, muonekano, mali, eneo au sehemu;
(b) umri wa jengo;
(c) muundo wa kisanifu wa jengo;
(d) matumizi ya urithi; na
(e) sera na miongozo ya Halmashauri;

Vibali vya Kuboresha Urithi

9. Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa anaruhusiwa kutoa vibali vya kuboresha urithi kwa:

(a) mali ya urithi iliyolindwa;
(b) mali ndani ya eneo la hifadhi ya urithi, ikiwa matumizi ya kibali yanahusiana na muonekano au tabia zilizotambuliwa katika Mpango wa Usimamizi wa Uhifadhi kama unavyochangia katika tabia ya urithi au thamani ya urithi ya eneo; na
(c) mali inayohusu makubaliano ya urithi revitalization au makubaliano ambayo yanahitaji kibali cha kuboresha urithi kipatikane.

Upataji wa vibali vya kuboresha urithi kwa mali ya urithi iliyoainishwa

10. Kwa kuzingatia masharti mengine ya sheria hii, mtu hatafanya lolote kati ya yafuatayo kwa mali iliyoainishwa kabla ya kupata kibali cha kuboresha urithi:

(a) kubadili upande wa nje wa jengo ambalo ni mali ya urithi iliyoainishwa;
(b) kufanya mabadiliko ya muundo wa jengo la mali ya urithi iliyoainishwa;
(c) kubadili, kuondoa au kuchukua hatua ambayo ingeweza kuharibu muonekano wa kisanifu au zana zilizowekwa mahali pa kudumu za usanifu za ndani ambazo ni mali ya urithi iliyoainishwa;
(d) kubadili, kuondoa au kuchukua hatua ambayo ingeweza kuharibu muonekano ambao ni mali

ya urithi iliyoainishwa; au

(e) kubadili, kuchimba au kujenga katika ardhi ambayo ni mali ya urithi iliyoainishwa.

Shughuli zisizohitaji kibali cha maboresho

11. Licha ya masharti ya sheria hii, kibali cha kubadili urithi hakihitajiki katika eneo la hifadhi ya urithi na mali ya urithi iliyohifadhiwa kwa:

(a) upakaji rangi wa majengo au miundo, ikiwa rangi zinazopendekezwa ni sawa na zilizopo;

(b) mabadiliko ya ndani ya jengo au muundo ambayo hayaongezi eneo la sakafu;

(c) matengenezo ya jengo ya kawaida; na

(d) matengenezo ya bustani ya kawaida.

Masharti ya Kibali cha Kuboresha Urithi

12. Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa anaruhusiwa kutoa vibali vya kubadili urithi kwa kuzingata vigezo, matakwa au masharti kama, kwa maoni ya Mkurugenzi, yanaendana na dhumuni la uhifadhi wa urithi wa mali kwa masharti masharti yafuatayo:

(a) kuheshimu mlolongo na muda wa ujenzi;

(b) kuheshimu tabia za mabadiliko au kitendo kitakachoidhinishwa, ikijumuisha mandhari ya eneo, muundo, umati, muonekano wa nje, nyenzo na umaliziaji wa jengo na muonekano wa mandhari ya nchi;

(c) kuheshimu mlolongo na muda wa umiliki; na

(d) kutaka kwamba muombaji atoe dhamana kwa mujibu wa Sheria hii.

Kushindwa kufuata masharti au kibali cha kuboresha urithi

13. Ikiwa, kwa maoni ya Mkurugenzi wa Makumbusho, mmiliki aliyepewa kibali cha kuboresha urithi ameshindwa kufuata kigezo, matakwa au sharti la kibali, Mkurugenzi wa Makumbusho anaweza kuwasilisha suala kwa Bodi akiomba: -

(a) kufanya uamuzi kama mwenye kibali cha kuboresha urithi ameshindwa kufuata kigezo, matakwa au sharti la kibali; na

(b) kutekeleza na kukamilisha ujenzi unaohitajika kuridhisha kigezo, matakwa au masharti au kurekebisha athari za ukiukwaji au kutokufuatwa, kwa gharama za mwenye kibali.

Kukataliwa kwa kibali cha kuboresha urithi

14. Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa anaweza kukataa kutoa kibali cha kubadili urithi ikiwa, kwa maoni ya Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa, kitendo pendekezwa kilichoidhinishwa hakitalingana na dhumuni la uhifadhi wa urithi wa mali, na kwa kufanya uamuzi huo, Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa anaweza kuzingatia vigezo vifuatavyo:

(a) kama muombaji ameshindwa kuwasilisha tathmini ya madhara alivyoamrishwa kufanya hivyo;
(b) kama muombaji ameshindwa kufuata vigenzo vilivyoainishwa katika taarifa ya tathmini ya madhara;
(c) kama kitendo pendekezwa kingepunguza thamani ya urithi au tabia ya urithi wa mali ya urithi iliyohifadhiwa au mali katika eneo la hifadhi ya urithi, na, katika kufanya uamuzi huo, Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa anaweza kuzingatia vigezo vya sheria hii; na
(d) kama mali inaongozwa na sheria ndogo inayotangaza kipindi cha udhibiti wa urithi.

Utoaji wa Kibali cha Maendeleo

15. Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa anaweza kuidhinisha kutolewa kwa vibali vya maendeleo kwa kuzingatia vigezo, matakwa au masharti hayo ambayo yanalingana na madhumuni ya maendeleo katika eneo la uhifadhi.

Kukataliwa kwa kibali cha maendeleo

16. Mkurugenzi anaweza kukataa kutoa kibali cha maendeleo ikiwa kwa maoni yake, kitendo pendekezwa kitapunguza thamani ya urithi au tabia ya urithi wa mali

ya urithi iliyohifadhiwa na katika kufanya uamuzi huo, Mkurugenzi anaweza kuzingatia vigezo vilivyoainishwa katika Sheria hii.

Kuzuia idhini

17. Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Mkurugenzi anaweza kuzuia idhini ya kibali cha maendeleo au kibali cha kubadili urithi ikiwa, kwa maoni yake kitendo pendekezwa kingebadili au kusababisha kubadilishwa kwa:

(a) mali ya urithi iliyolindwa;
(b) mali inayopewa uhifadhi wa urithi wa muda; au
(c) mali katika rejesta ya urithi.

Taarifa ya kuzuia idhini kwa muombaji

18. Ikiwa Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa anazuia kibali cha maendeleo au kibali cha kubadili urithi kwa mujibu wa masharti ya Sheria Ndogo hii, atamtaarifu Muombaji kwa maandishi:

(a) sababu za kuzuia idhini; na
(b) ikiwa hajaridhika na uamuzi anaweza kukata rufaa kwa Bodi;

Kikomo cha kuzuia idhini

19. Bila kuathiri masharti ya kanuni ya 18 Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa hatazuia idhini ikiwa muombaji anakubaliana na vigezo na masharti ya Halmashauri baada ya kuridhika kwa Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa kuzuia au kupunguza mazingira ambayo yanaweza kupunguza thamani ya urithi au tabia ya urithi ya mali.

Rufaa kwa Bodi

20. Mmiliki au muombaji kibali anaweza kukata rufaa kwa Bodi kwa uamuzi uliofanywa na Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa kuhusiana na:

(a) kukataa kutoa kibali cha maendeleo ndani ya eneo la uhifadhi kwa mali ya urithi iliyohifadhiwa;
(b) utoaji au kukataliwa kwa kibali cha kuboresha

urithi;

(c) uamuzi kama matakwa na masharti ya kibali cha kuboresha urithi yamefikiwa;

(d) kwa kuwasilisha ombi la maandishi kwa Bodi ndani ya siku 14 za uamuzi, likianisha sababu za ombi.

Uamuzi wa rufaa

21. Bodi itaamua rufaa ndani ya muda unaofaa, na inaweza kukubaliana au kutengua uamuzi.

Amri ya Ukaguzi wa Urithi

22.-(1) Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa anaweza kutoa amri ya ukaguzi wa urithi katika mazingira yafuatayo:

(a) endapo utakuwa katika hatari ya kuzorota au kuharibika kutokana na kushindwa kukarabati au kurekebisha mali;

(b) ametaarifiwa kwamba ujenzi unafanyika bila kibali;

(c) kuna shughuli zisizohalali zinaendelea; au

(d) sababu au mazingira mengine yoyote itakapolazimu.

(2) Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa atachukua hatua atakapoona inafaa za kumtaarifu mmiliki au mkaaji kabla ya au baada ya kuingia katika ardhi au jengo na atawasilisha nakala ya amri kwa mmiliki au mkaaji.

Watu wanaoruhusiwa kuingia katika eneo la uhifadhi

23-(1) Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa au Afisa Mwidhiniwa wanaruhusiwa kuingia katika ardhi au jengo katika muda wowote wa kazi kuhakikisha uzingatiwaji wa Sheria hii au sheria nyingine yoyote.

(2) Wanaweza kuchukua hatua stahiki za kumtaarifu mmiliki au mkaaji kabla ya au baada ya kuingia katika ardhi au jengo; na

(3) Endapo kuna uvunjwaji wowote wa Sheria hii, Mkurugenzi atachukua hatua za muhimu na sahihi

ikijumusha kuitaarifu mamlaka husika.

Vipimo na Sampuli

24. Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa anaidhinishwa kufanya vipimo na kuondoa nyenzo za sampuli ambazo, kwa maoni yake ni muhimu kwa dhumuni la ukaguzi wa urithi, isipokuwa kwamba anaweza kuhakikisha kwamba mabadiliko yoyote yaliyosababishwa na vipimo hivyo ni madogo na hayaonekani kwa kadri inavyowezekana ukizingatia matakwa ya ukaguzi wa urithi.

Taarifa kwa mmiliki

25. Kufuatia kukamilika kwa ukaguzi wa urithi, Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa:

(a) atamtaarifu mmiliki juu ya ukaguzi wa urithi; na

(b) atamtaarifu mmiliki ikiwa mabadiliko yoyote yamefanyika au nyenzo kuondolewa wakati wa ukaguzi wa urithi.

Tathmini ya Madhara

26. Ikiwa, kwa maoni ya Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa, idhini chini ya sheria hii au sheria nyingine inaweza kuathiri mali ya urithi iliyolindwa, anaweza kumtaka muombaji wa idhini:

(a) kutoa kwa Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa tathmini ya athari, kwa gharama za muombaji; au

(b) kumruhusu Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa kufanya tathmini ya athari.

Tathmini ya Athari ya Urithi wa Kiutamaduni kufanywa na Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa

27. Tathimini ya athari ambayo inafanywa na Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa ni lazima:

(a) ifanyike kwa usahihi; na

(b) ifanyike kwa gharama za Makumbusho ya Taifa.

Taarifa ya Tathmini ya

28. Taarifa au amri ya Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa kwa mujibu wa Sheria ya

Athari ya Urithi wa Kiutamaduni

Usimamizi wa Mazingira:

(a) itakuwa kwa maandishi na itaelekezwa kwa muombaji wa idhini; na

(b) itajumuisha mtungamano ufuatao:

(i) taarifa ambayo ni lazima itolewa katika tathmini ya athari, na

(ii) taaluma za muhimu za mtu au watu wanaofanya utafiti kuandaa tathmini ya madhara.

Mabadiliko ya mtungamano

29. Mtungamano katika taarifa au amri ambayo imetolewa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na inaweza tu kubadilishwa na Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa kwa idhini ya mmiliki au muombaji.

Uchambuzi wa Tathmini ya Athari ya Urithi wa Kiutamaduni

30. Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa anaruhusiwa kuamua kama mtungamano uliojumuishwa katika taarifa au amri kuhusiana na tathmini ya madhara umefikiwa.

Makosa na Adhabu

31. Mtu yeyote atakayethibitika kuwa amevunja au kwenda kinyume na masharti ya Sheria hii atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote kwa pamoja, yaani faini na kifungo.

Lakiri ya Halmashauri ya manispaa ya Mtwara- Mikindani imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufutia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika Tarehe 07 mwezi, Oktoba, Mwaka 2022 mbele ya ;-

MWL. HASSAN. B. NYANGE
*Mkurugenzi wa Manispaa*
*Mtwara- Mikindani*

MHE. SHADIDA ALLY NDILE
*Mstahiki Meya wa Manispaa*
*Mtwara -Mikindani*

NAKUBALI

L.S

Dodoma,
2 February, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
*Waziri wa Nchi- Ofisi ya Rais*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*